# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

# MLIMANI SACCOS LIMITED

**S.L.P 35091, DAR ES SALAAM**

## *SERA YA MIKOPO*

***Kukopa ni haki ya msingi ya Mwanachama na kurejesha ni wajibu wake***

**June 2012**

**YALIYOMO**

1. UTANGULIZI …………………………………………………………..3

2. KAMATI YA MIKOPO………………………………………………3

3. AINA YA MIKOPO…………………………………………………….3

4. MKOPO WA MAENDELEO…………………………………….….3

5. MKOPO WA DHARURA……………………………………..……..4

6. MKOPO WA ELIMU………………………………..……………4

7. MKOPO WA MAZISHI………………………………………………..5

8. UDHAMINI NA MASHARTI YAKE…………………………………5

9. USIMAMIZI WA MIKOPO……………………………………………6

10. ADHABU KWA UKIUKWAJI WA MASHARTI YA MIKOPO…….7

11. KINGA DHIDI YA  MAJANGA……………………….…………...7

12. MENGINEYO……………………………………………………..…8

## 1. UTANGULIZI

Sera ya Mikopo ya Mlimani SACCOS imeandaliwa na Bodi kwa lengo la kukidhi mahitaji ya kanuni za Chama. Hata hivyo, utekelezaji wake unapaswa kuidhinishwa na Mkutano Mkuu. Sera hii ndiyo mwongozo kwa kila mkopo ambao mwanachama atauomba ili aweze kuwajibika katika nafasi yake kama mkopaji. Bodi ya chama ndiyo itakayokuwa na kauli ya mwisho katika mkopo wowote ulioanishwa kama ilivyotamkwa ndani ya sera hii.

## 2. KAMATI YA MIKOPO

Kamati ya Mikopo itaundwa na Wajumbe watatu (3) watakaotokana na Wajumbe wa Bodi ya Kipindi husika waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Chama. Kamati hii itatoa mikopo kulingana na vigezo vilivyowekwa yaani: Mshahara wa mwombaji mkopo, wadhamini na dhamana. Pia, itakuwa na jukumu la kuhakikisha wanachama wanapata mikopo na wanairejesha kwa wakati, na kufuatilia wadaiwa sugu.

## 3. AINA YA MIKOPO

Chama cha kuweka na kukopa cha Mlimani kitakuwa na mikopo ya aina zifuatazo:-

(i) Mkopo wa Maendeleo.

(ii) Mkopo wa dharura.

(iii) Mkopo wa Elimu

(iv) Mkopo wa Mazishi

## 4. MKOPO WA MAENDELEO

(i) Mkopo huu ni wa kawaida na marejesho yake ni miezi thelathini na sita (36). Pia, huu ni mkopo ambao huchukuliwa na mwanachama kwa lengo la kuanzisha kitu cha manufaa katika maendeleo yake ya kila siku.

(ii) Mkopo wa Maendeleo utakopwa si zaidi ya mara tatu ya Akiba alizowekeza mwanachama katika chama na italipwa kwa riba iliyoinishwa na Mkutano Mkuu kwa wakati huo.

(iii) Mwanachama anayo fursa ya kuchagua muda wa kurejesha kwa muda mfupi chini ya miaka mitatu ili mradi amalize deni mapema na aweze kukopa tena. Kwa kuwa ni mkopo wa maendeleo, Mwanachama hanabudi kukopa ili kujiletea maendeleo yake binafsi ikiwa anakidhi vigezo vilivyoainishwa hapo juu. Kamati ya Mikopo itakutana mara moja tu kwa mwezi kupitisha mikopo hii.

(iv) Mkopo huu hautakiwi kuzidi Shilingi za Kitanzania Milioni Ishirini (20,000,000/=) bila kujali akiba za mkopaji.

(v) Mkopo huu utatozwa riba ya asilimia 1.4

## 5. MKOPO WA DHARURA

(i) Mkopo huu utakopwa kwa kiwango kitakachopangwa na bodi kwa wakati huo na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu na utarejeshwa kwa kipindi cha miezi minne (4) pamoja na riba iliyopitishwa na Mkutano Mkuu. Hata hivyo mwanachama anayofursa ya kurejesha chini ya miezi minne. Mikopo hii itatolewa kwa utaratibu utakaopangwa na Kamati ya Mikopo.

(ii) Mkopo huu hautazidi Shilingi Laki Nne (400,000/=) ilimradi kipato cha mkopaji kinatosheleza.

(iii) Mikopo ya dharura itakuwa kwa matatizo kama yafuatayo:-

(vi) Kubomokewa na makazi

(vii) Faini za mahakamani

(viii) Ajali yeyote

(ix) Gharama za tiba

(x) Tatizo jingine lolote litakalohitaji pesa ya haraka

(xi) Mkopo huu utatozwa riba ya asilimia mbili (2%)

**6. MKOPO WA ELIMU**

(i) Mkopo huu utatolewa hata kama mwombaji ana mikopo ya aina nyingine ili mradi mshahara wake unaweza kurejesha kulipa mkopo huu katika kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili (12)

(ii) Mkopo wa Elimu ni kwa ajili ya Shule za ndani na nje ya Tanzania

(iii) Mkopo huu utatozwa riba ya asilimia mbili (2%)

**7. MKOPO WA MAZISHI**

(i) Mkopo wa mazishi unamadhumuni ya kuwawezesha wanachama kushughulikia masuala ya mazishi kwa kutoa mkopo usiozidi Tshs. 500,000/= ambao utarejeshwa katika kipindi cha mwaka mmoja. Riba itakayotozwa ni ile itakayokuwa inatumika kwa wakati huo.

(ii) Mkopo huu utatolewa kwa Mwanachama ambaye amefiwa na aidha baba, mama, mume, mke au mtoto.

**8. UDHAMINI NA MASHARTI YAKE**

(i) Mwanachama anayeomba mkopo lazima ajaze fomu atakayoilipia Tshs. 3000/=. Kwa mkopo wa maendeleo na 2000/= kwa mikopo mingineyo. Pesa hii itaingia kwenye mfuko wa chama na hairudishwi.

(ii) Mkopo wa Elimu, Dharura na Mazishi itadhaminiwa na akiba za mkopaji na bima ya Ndani.

(iii) Mwanachama haruhusiwi kudhamini zaidi ya mikopo mitatu. Wadhamini wote lazima wawe wanachama.

(iv) Makato kwa marejesho ya mkopo yataanza mara moja bila kuzidi mwezi mmoja baada ya mkopo kutolewa.

(v) Kigezo kikubwa cha kuamua uwezo wa Mwanachama kupewa mkopo ni mshahara wake halisi na mapato mengineyo.

(vi) Mwanachama yeyote hataruhusiwa kupunguza Akiba zake wakati ana mkopo isipokua anapo acha uanachama. Mwanachama atarejeshewa akiba yake pamoja na hisa ikiwa tu hana deni lolote ndani ya chama. Endapo anadaiwa akiba yake pamoja na hisa vitatumika kulipa deni.

(vii) Suala la Udhamini ni suala la lazima na kila mwanachama anashauriwa azingatie hilo kwa mujibu wa sheria ya Ushirika ya mwaka 2003.

(viii) Wadhamini wote lazima wawe wanachama wa Mlimani Saccos.

(ix) Wajibu wa mdhamini utaisha pale tu nafasi yake itakapochukuliwa na mdhamini mwingine aliyekubalika na Chama, pia udhamini utakoma pale ambapo deni lililodhaminiwa limelipwa lote.

(x) Kumbukumbu za wadhamini zitatunzwa katika faili la kila mkopaji.

(xi) Gharama za ukaguzi wa dhamana za mali zisizo hamishika zitalipwa na mwombaji.

**9. USIMAMIZI WA MIKOPO**

(i) Chama hakitaruhusu mwanachama kuchukua mkopo ambao marejesho yake yatazidi muda uliopangwa.

(ii) Mwenyekiti na Wajumbe wa bodi hawaruhusiwi kuingilia kazi za kawaida za Kamati ya mikopo.

(iii) Mwanachama anaruhusiwa kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa kamati ya mikopo kwa Bodi, endapo ataona hakutendewa haki na Kamati hiyo.

(iv) Wakati wa kusikiliza rufaa ya huyo mwanachama wajumbe wa Kamati ya mikopo hawatakuwa na kura.

(v) Fedha inayolipwa taslimu nje ya utaratibu wa kawaida wa makato kwa madhumuni ya kutunisha akiba hazitafikiriwa kwa mkopo hadi zikae chamani kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu.

(vi) Mikopo itatolewa kwa wanachama tu.

(vii) Mwanachama anayeomba likizo bila malipo kwa mwajiri na anadaiwa na Chama atawajibika kufanya yafuatayo:-

a. Kulipa deni lote au
b. Kulipa kiwango na makato ya kipindi ambacho atakuwa likizo bila malipo.

## 10. ADHABU DHIDI YA UKIUKWAJI WA MASHARTI YA MIKOPO

i) Hakuna Mwanachama atakaye ruhusiwa kujiondoa ndani ya Chama iwapo hajalipa madeni yake yote, isipokuwa pale ambapo akiba na hisa zake zinaweza kutumika kulipa hilo deni.

ii) Hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mwanachama atakaye kwenda kinyume na taratibu za vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa ikiwa ni pamoja na kumfuta uanachama mtu ambaye atakuwa na tabia zinazoenda kinyume na sheria za kazi.

iii) Mwanachama atatozwa faini kwa cheleweshо la mkopo huu kwa asilimia 5%.

## 11. KINGA DHIDI YA MAJANGA

(i) Mlimani Saccos kitakuwa ni mwanachama wa Kinga ya Majanga iliyo chini ya

SCCULT ambayo itakuwa ikichangiwa na Chama na wanachama kwa mikopo ya Maendeleo. Michango inayotolewa ili kukinga mikopo hiyo itatengewa fungu lake la kinga ya majanga kwenye bajeti kila mwaka wa fedha wa Chama na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa wanachama.

(ii) Mwanachama atakatwa kiasi cha asilimia 1.5% ya mkopo wake kama kinga dhidi ya majanga. itakayopitishwa na Mkutano Mkuu.

(iii) Chama kitakuwa na fursa ya kutoa rambi rambi kwa mwanachama wake pindi akifariki kwa kiwango cha Tshs. 100,000/= . Kiwango hiki kitakuwa kinarekebishwa kulingana na muda na wakati wa kuidhinishwa na Mkutano Mkuu.

**12. MENGINEYO**

(i) Sera hii inawekwa mahususi ili kila mwanachama ajue wajibu, kazi na majukumu yake. Hivyo inatarajiwa kuwa iwapo haya yaliyoelezwa ndani ya sera hii yatatekelezwa ipasavyo Chama kitajiweka katika hali nzuri ya uendeshaji wa shughuli zake za kila siku.

(ii) Mwongozo wa Sera hii ni sheria ya ushirika ya Mwaka 2003, kanuni za ushirika za 2004 na Masharti ya Chama.

(iii) Sera hii ya mikopo itaenda sambamba na kanuni ya fedha ili fedha yeyote inayoidhinishwa iwe ndani ya utaratibu wa sheria ya fedha.

(iv) Endapo patatokea haja ya kuboreshwa Sera hii, hoja itafanywa na Bodi ya Chama na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa wanachama.